

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



MTIHANI WA MUHULA WA PILI MKOA WA IRINGA – 2023

KIDATO CHA KWANZA

KISWAHILI

021

Muda: 2:30 Saa

Jumamatu, 20 Novemba 2023

Maelekezo

- Jibu maswali kulingana na maelekezo ya sehemu husika

MsomiBora.com

SEHEMU A: (alama 16)

1. Jibu maswali yote yafuatayo
 - i. Kila lugha katika mawasiliano hutumia mfumo ili mawasiliano yaeleweke. Miongoni mwa maneno yafuatayo, chagua mfumo ulio sahihi katika kuwasiliana.
 - A. Lugha, mawasiliano, ujumbe, mtoa ujumbe, media, mpokeaji na mrejesho.
 - B. Mpokea ujumbe, ujumbe, mawasiliano na mrejesho.
 - C. Mtoa ujumbe, ujumbe, media, mpokea ujumbe na mrejesho.
 - D. Media, mpokeaji, mrejesho, ujumbe na mtoaji.
 - ii. Zifuatazo ni dhima za lugha katika mawasiliano kasoro:
 - A. Kutambulisha utamaduni.
 - B. Kupashana habari.
 - C. Kutunza historia.
 - D. Kukaa maneno.
 - iii. Kiimbo hufasiliwa katika mazungumzo kuwa
 - A. Kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji.
 - B. Mawimbi ya sauti wakati wa kuzungumza.
 - C. Kuzungumza kwa kutumia mawimbi ya sauti.
 - D. Yote hapo juu ni sawa.
 - iv. Chagua sentensi moja kati ya hizi zifuatazo kuwa haina maana zaidi ya moja :
 - A. Nipe sahani ya kulia.
 - B. Kaka amefua nguo.
 - C. Jenro amenunua mbuzi.
 - D. Mama anakanga.
 - v. Dhana ipi kati ya hizi zifuatazo huonesha utambulisho wa mzungumzaji :
 - A. Sauti.
 - B. Silabi.
 - C. Matamshi.
 - D. Lafudhi.
 - vi. Mpira upo chini ya mti. Neno chini ya ni aina gani ya neno ?
 - A. Kitenzi kishirikishi.
 - B. Kivumishi.
 - C. Kihusishi.
 - D. Kiunganishi.
 - vii. Kila aina ya tangazo hutolewa na mtangazaji, wasikilizaji hupata habari kutoka kwa mtangazaji. Je, katika fasihi kazi hiyo huwasilishwa na nani kati ya hawa wafuatao :
 - A. Wasikilizaji.
 - B. Fanani.
 - C. Waandishi.

- D. Wazungumzaji.
- viii. Taja tofauti ya msingi kati ya mashairi na ngonjera :
- A. Mpangilio wa maneno.
- B. Mpangilio wa vina na mizani.
- C. Mpangilio wa kimziki na kiridhimu.
- D. Majibizano baina ya watu wawili au zaidi.
- ix. Mtunzi wa kazi ya fasihi hujitahidi kufikisha mawazo makuu kwa walengwa kwa njia ya;
- A. Dhamira.
- B. Maudhui.
- C. Falsafa
- D. Fani.
- x. Katika uhalisia unaomtofautisha muwasilishaji wa kazi za fasihi na mwingine huwa katika kigezo cha:
- A. Maudhui.
- B. Fani.
- C. Mtindo.
- D. Muundo.

Majibu

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

2. Oanisha kauli katika orodha “A” kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka B

ORODHA A	ORODHA B
i. Soga	A. Husimulia matukio mbalimbali ya kihistoria.
ii. Methali	B. Husimulia pich ana mafumbo zinazoonesha ukinzani wa fikra au tukio.
iii. Tarihi	C. Huonesha pande mbili zenye fikra katika usimuliaji kwa kuoa hekima na busara.
iv. Hadithi	D. Husimuliwa kwa nia ya kufurahisha na kukejeli.
v. Visasili	E. Husimulia vyanzo na asili ya jambo au kitu Fulani.
vi. Mizungu	F. Ni vikundi vidogo vidogo vy tanzu
	G. Ni masimulizi marefu yanayohusisha visa na matukio.

Majibu

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.

Sehemu B (ALAMA 54)

Jibu maswali yote

3. Andika ‘K ‘ kwa kisemo cha kweli na ‘S’ kwa kisemo kisicho cha kweli kwenye sentensi zifuatazo

- i. Utoaji na upokeaji ujumbe hutumiwa na fani na hadhira.....
- ii. Mrejesho wa ujumbe ni miongoni mwa vipengele vinavyotumika katika mchakato wa mawasiliano.....
- iii. ‘Mpendwa mama shikamoo, wote wazima?’ Hii ni sentensi inayotambulisha salamu au mwanzo wa barua ya kirafiki.....
- iv. Redio ni kifaa kimojawapo kati ya vifaa visivyo toa taarifa katika jamii.....
- v. Ufahamu wa kuona ni kati ya aina za ufahamu katika lugha ya kiswahili.....
- vi. Mlinzi hulinda ndege,mke mzuri halindwi.....
- vii. Lakuvunda lina ubani pema.....
- viii. Mwenye kukataa pema, pabaya hapamkonyezi.....
- ix. Werevu mwingi mbele mwanga.....

4. Malizia methali zifuatazo ili ziweze kutoa mafunzo na maadili mema :

- a) Ada ya mja hunena.....
- b) Bahari iliko.....
- c) Chovya chovya.....
- d) Daraja lisilokuvusha.....
- e) Eneo la kiwanja si hoja.....
- f) Fisi akiwa hakimu.....
- g) Ganga ganga ya mganga.....
- h) Kamba ya mbali.....
- i) Msema kweli.....

5. Eleza kwa kutoa mifano tofauti iliyopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. (Toa hoja nne)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

6. Kwa kuzingatia lafudhi na matamshi sahihi, Bainisha maneno yenye makosa na ziandike upya sentensi hizo.

a) Hata wenzetu waliosoma huendaga mjini.

.....

b) Nimepata ujumbe wenye taharifa mbaya.

.....

c) Kurara badala ya kufanya kazi kunasababisha maisha kuwa magumu.

.....

d) Ama kweri erimu haina mwisho.

.....

e) Rafiki yangu naja.

.....

f) Ntoto wangu aumwa.

.....

7. a) Toa tofauti kati ya sentensi zifuatazo kisha ziwekee vipaumbele kwa kila sentensi.

b) Tenganisha maneno yafuatayo kwa silabi kwa kuweka idadi ya silabi

i. Shusha

ii. Gharama.....

iii. Kiswahili.....

c) Toa utata katika neno **KATA** kisha andika sentensi upya.

.....

.....

8. Tunga sentensi zenye miundo ifuatayo kwa kutumia maneno haya

i. N + T_s + T + N + E

.....

.....

ii. N + V + T + E

.....

.....

iii. W + V + T_s + T + H + N

.....

.....

iv. W + t + N + V

.....

.....

Section C (ALAMA 30)

Jibu maswali mawili tu kutoka sehemu hii. Swali la 9 ni la lazima

9. Hakiki shairi lifuatalo kwa kutumia vigezo hivi.

1. Karudi baba mmoja, toka safari ya mbali,
Kavimba yote mapaja, na kutetemeka mwili,
Watoto wake wakaja, ili kumtaka hali,
Wakataka na kauli, iwafae maishani.

2. Akatamka mgonjwa, ninaumwa kweli kweli
Hata kama nikichanjwa, haitoki homa kali,
Roho naona yachinjwa, kifo kinanikabili,
Semeni niseme nini, kiwafae maishani.

3. Wakazidi kumchimba, baba mwenye homa kali,
Baba yetu watufumba, hatujui fumbo hili,
Akili zetu nyembamba, hazijajua methali,
Kama tunataka mali, tutapataje shambani.

Maswali

a) Pendekeza jina la Shairi lililoandikwa hapo juu.

.....

b) Bainisha wahusika waliojitokeza kutoka katika shairi hili.

.....

.....

.....

c) Bainisha vina na mizani kutoka beti wa kwanza.

.....
.....
.....

d) Kwa kutoa mifano, bainisha dhamira mbili na ujumbe mmoja kutoka katika shairi hili.

.....
.....
.....
.....
.....

e) Kila ubeti umetumia mistari mingapi ? Na kwa ujumla mishororo hiyo huitwa.....(Toa sababu)

.....
.....
.....
.....
.....

f) Eleza vituo vilivyotumika katika shairi hili.

.....
.....
.....
.....
.....

10. Andika insha kati ya mada zifuatazo :

- a) Misitu.
- b) Madawa ya kulevya.
- c) Athari za ugonjwa wa ukimwi.

11. a) Jifanye wewe ni mwanafunzi wa kidato chan nne(4) unayetarajia kuhitimu baada ya mitihani ya mwisho. Mwandikie mama yako barua kuomba akusaidie kubeba mizigo. Jina lako liwe Neema Wageni wa S.L.P 500 Mbeya.

b) Andika mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandika barua ya kirafiki

This image shows a full page of a document template. It consists of approximately 30 evenly spaced horizontal dotted lines across the entire width of the page, providing a guide for handwriting or typing. There are no margins, text, or other markings present.

This image shows a full page of white paper with horizontal dotted lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page, providing a guide for handwriting practice. There are no margins, text, or other markings on the page.